**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

# TANGAZO KWA UMMA

Wizara ya Katiba na Sheria kwa mujibu wa Kanuni za Ithibati ya Waendesha Maridhiano, Majadiliano, Upatanishi na Usuluhishi, 2021 (Reconciliation, Negotiation, Mediation and Arbitration (Practitioners Accreditation Regulations, 2021) imepewa mamlaka ya kusajili Waendesha Maridhiano, Majadiliano, Upatanishi na Usuluhishi ambao wanakidhi vigezo kwa mujibu wa Kanuni husika.

Hivyo, Wizara inapenda kuwatangazia Watoa Huduma za Usuluhishi, Upatanishi, Uendeshaji wa Maridhiano na Majadiliano ambao wamekidhi vigezo kuwasilisha maombi yao kwa kujaza Fomu ya Maombi Na. TAF1 na kuwasilisha nyaraka na viambatisho kupitia mfumo kiungo https://mmuu.sheria.go.tz/register. Kwa ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na Ofisi ya Msajili kupitia msajili.mmuu@sheria.go.tz au Simu **Na. 0262160360.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **30 Machi, 2025**.

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**
**06 Machi, 2O25**